**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**652** **ELIMU KWA MICHEZO**

**Muda: Saa 3.** **Mwaka : 2013**

---

**MAELEKEZO.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C** yenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu **B** and **C**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na sehemu **B** na **C** zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Vikokotozi **haviruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (40 Alama)

Jibu maswali yote katika sehemu hii

1. Eleza maana ya rasilimali watu katika michezo na taja mifano yake.

2. Taja michezo minne ya asili na eleza umuhimu wake katika malezi ya kijamii.

3. Fafanua hatua nne zinazofuatwa wakati wa kufunga goli kwa kichwa katika mpira wa miguu.

4. Bainisha sheria nne muhimu katika mchezo wa badminton.

5. Eleza stadi nne za msingi zinazotumika katika mpira wa kikapu.

6. Eleza faida nne walizopata vijana waliojishughulisha na kuandaa mashindano ya michezo katika jamii zao.

7. Changanua stadi nne zinazohitajika katika mchezo wa mikono ili kuongeza ufanisi wa timu.

8. Eleza faida nne za kutumia mitandao ya kijamii katika kukuza michezo.

9. Eleza mambo manne muhimu ya kuzingatia kabla ya kuandaa mashindano ya ligi ya kanda.

10. Changanua njia nne za mawasiliano ya moja kwa moja kati ya wachezaji na waamuzi uwanjani.

## SEHEMU B (30 Alama)

Jibu maswali mawili katika sehemu hii

11. Tathmini nafasi ya michezo katika kulinda na kuendeleza afya za jamii.

12. Eleza hatua tano za msingi za kumpatia huduma ya kwanza mwanafunzi aliyeumia bega wakati wa mchezo.

13. Changanua mifumo mitatu ya kawaida ya wachezaji katika mpira wa miguu □ae leza udhaifu wake.

## SEHEMU C (30 Alama)

Jibu maswali mawili katika sehemu hii

14. Eleza kanuni sita za usalama zinazopaswa kuzingatiwa katika michezo ya maji.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

15. Jadili changamoto zinazojitokeza katika utawala wa michezo ya shule na njia za kuzitatua.

16. Kwa mifano, eleza nafasi ya michezo katika kutangaza utalii wa nchi.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org